www.global-minbar.com/sw

# [1] FADHILA YA KUDUMU KATIKA TAWHIDI (KUMPWEKESHA MWENYEZI MUNGU)

## Lengo la Khutba:

1. Kubainisha umuhimu wa Tawhidi na Fadhila zake.
2. Kubainisha kwamba Tawhidi ni sababu ya kuokoka mwanadamu Siku ya Kiama na kupata msamaha wa dhambi.
3. Kubainisha kwamba Tawhidi ni sababu ya kuondosha balaa na fitna.
4. Kubainisha umuhimu wa kujifundisha Tawhidi, na Shirki kwa aina zake.

## KHUTBA YA KWANZA

## Utangulizi

Shukrani za dhati ni kwa Mola Mkarimu. Rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad. Tutazungumzia katika khutba hii mambo yafuatayo:- kubainisha umuhimu wa Tawhidi na fadhila zake, kubainisha kwamba Tawhidi ni sababu ya kuokoka mwanadamu siku ya kiama na pia kubainisha kwamba Tawhidi ni sababu ya kuondoshewa balaa na fitna vile vile nibainishe umuhimu mkubwa wa kujifundisha Tawhidi na shirki kwa aina zake.

Ama baada ya haya, Tawhidi ni msingi mkubwa ambao Mwenyezi Mungu amewaumba majini na watu kwa ajili yake. Kwani Mwenyezi Mungu hakuwaumba majini na watu isipokuwa kwa kumuabudu yeye.

قال تعالى : ﴿وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾﴾ [الذاريات : ٥٦] .

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala) : {{Sikuwaumba majini na watu isipokuwa waniabudu}} [Addhariyati : 56].

Ndugu katika imani na wausia kumcha Mwenyezi Mungu kwa siri na kwa dhahiri na jueni ya kwamba moyo wa Muislamu hauwi mzuri isipokuwa kwa Tawhidi. Kwani Tawhidi ni jambo kubwa. Allah (Subhaanahu wa Taala) Amelibainisha katika kitabu chake na pia Mtume, rehma na amani zimfikie ameliweka wazi katika hadithi zake tukufu.Tawhidi ni jambo ambalo hawezi kuokoka mtu yoyote duniani na kesho Akhera ila alikamilishe jambo hilo la kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kutomshirikisha na chochote. Amesema Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam): [Atakaye kufa na akijua ya kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu ataingia peponi].

## Umuhimu wa Tawhidi

1. Tawhidi ni jambo bora sana, na kwa sababu hii Allah (Subhaanahu wa Taala) Ameshuhudia kwa nafsi yake vile vile Malaika wameshuhudia na pia waliopewa ilimu. Na hii ni kuonesha ubora wa jambo hili la Tawhidi. Jambo Amelishuhudilia Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala), wakashuhudia Malaika watukufu na pia wanadamu watukufu na watu waliopewa ilimu.



www.global-minbar.com/sw

قال تعالى : ﴿ شَهِدَ ٱللَّهُ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَأُو۟لُوا۟ ٱلْعِلْمِ قَآئِمًۢا بِٱلْقِسْطِ ۚ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ ﴿١٨﴾ ﴾ [آل عمران : ١٨].

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): {{Ameshuhudia Mwenyezi Mungu ya kwamba hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye na Malaika na pia waliopewa ilimu,hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye Mwenye nguvu Mwenye hekima}} [Al-Imran : 18 ].

2. Miongoni mwa umuhimu wa Tawhidi ni kwamba Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Alilingania Tawhidi kuanzia mwanzo wa ulinganizi wake hadi mwisho wa uhai wake, bali Mitume wote walilingania hivyo.
3. Pia tunapata katika sira ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) ya kwamba alipokuwa akituma maswahaba kwenda kulingania katika sehemu fulani huwausia kwanza kuwalingania Tawhidi.
4. Miongoni mwa umuhimu wa Tawhidi ni kwamba mwenye kushikamana na Tawhidi husamehewa dhambi zake na anaepushwa kukaa motoni.
5. Mwenye kushikamana na Tawhidi huwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu na pia hupata amani kamili na uongofu hapa duniani na kesho akhera.

قال تعالى : ﴿ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَلَمْ يَلْبِسُوٓا۟ إِيمَٰنَهُم بِظُلْمٍ أُو۟لَٰٓئِكَ لَهُمُ ٱلْأَمْنُ وَهُم مُّهْتَدُونَ ﴿٨٢﴾ ﴾ [الأنعام : ٨٢]

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Wale walioamini na wasichangane imani zao na dhulma watapata amani na wataongoka}} [Al-Anaam : 82]. Kwa mujibu wa Aya hii ni kwamba Muislamu anayeshikamana na Tawhidi atakuwa na amani hababaiki hapa duniani yuwajua litakalompata hapa duniani ni kadari ya Mola (Subhaanahu wa Taala) na kuwa atapata amani kesho akhera.

Bila ya kusahau kuwa endapo waumini watashikamana na tauhudi wataondoshewa balaa na fitna kesho akhera. Amesema Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam): [Anayeshuhudia ya kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye asiyekuwa na mshirika na Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na kwamba Nabii Isa ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na neno lake alilolitia kwa Mariam na roho kutoka kwake na pepo ni haki na moto ni haki Mwenyezi Mungu atamwingiza peponi kulingana na amali].

Ni vyema niwatajie mifano ya ambao waliepushiwa balaa na fitna.Tutoe mfano katika Mitume walioepushiwa balaa na fitna ni Nabii Ibrahiim pale walipokuwa watu wake wanataka kumchoma Mwenyezi Mungu Alimwokoa kwa kuuambia moto: “Ewe moto kuwa baridi na salama kwa Ibrahim” na ikawa kama alivyotaka Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Na Mtume mwengine ni Nabii Lut pale Mwenyezi Mungu Alipowaangamiza watu wake na kumwokoa yeye na waliomwamini yeye na mifano ya walioepushiwa balaa na fitna ni mingi na sababu ya kuepushiwa balaa ni kwa sababu ya kushikamana kwao na Tawhidi. Enyi waumin! Napenda kutaja bali kufafanua japokuwa kwa uchache aina za Tawhidi.

www.global-minbar.com/sw

www.global-minbar.com/sw

## Aina ya Tawhidi:

1. Tawhidi ya vitendo vya Mwenyezi Mungu nayo ni kumpwekesha Yeye katika uumbaji na uendeshaji wa mambo ya viumbe, na hashirikiani na yoyote katika hilo yoyote.

قال تعالى : ﴿ ٱللَّهُ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ وَأَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً فَأَخْرَجَ بِهِۦ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۖ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلْفُلْكَ لِتَجْرِىَ فِى ٱلْبَحْرِ بِأَمْرِهِۦ ۖ وَسَخَّرَ لَكُمُ ٱلْأَنْهَٰرَ ﴿٣٢﴾ ﴾ [إبراهيم ٣٢ ].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba mbingu na ardhi na ameteresha kutoka mawinguni maji akatoa kwa maji hayo mazao hali yakuwa ni riziki kweni nyinyi na akawadhalilishia majahazi ili yapite katika bahari kwa amri yake, na akawadhalilishia nyinyi mito ya maji} [Ibrahim: 32 ].

2. Tawhidi aina ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika ibada. Maana ya maneno haya ni kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye Anayefaa kuabudiwa.

قال تعالى : ﴿ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾ ﴾ [الفاتحة : ٥]

Asema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Ni wewe tu tunakuabudu na kwako wewe peke yako tunataka msaada}} [Al-Faatiha : 5].

3. Tawhidi ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika Sifa Zake na majina yake. Maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu hafanani na yoyote katika Sifa Zake na majina.Wala hafai yoyote kujifananisha wala kumfananisha yoyote na Mwenyezi Mungu katika sifa au majina yake kwani hana mfano wa yoyote.

قال تعالى : ﴿ قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ﴿٢﴾ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ﴿٣﴾ وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدٌۢ ﴿٤﴾ ﴾ [الإخلاص : ١ – ٤].

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): {{Sema; Mwenyezi Mungu ni mmoja Mwenyezi Mungu Ndiye Anayetakwa msaada, hakuzaa wala hakuzaliwa na Hana mfano Wake yoyote}} [Al-Ikhlas 1 - 4].

Aina zote za Tawhidi ni lazima kwa Muislamu azijue na azitumie katika maisha yake na hii ni kwa faida ya Muislamu. Na endapo mtu ataenda kinyume na aina hizi za Tawhidi basi ameshajitia matatizo duniani na kesho akhera, kwani Mwenyezi Mungu hamsamehe anayekufa katika shirki bila yakutubai**.**

قال تعالى : ﴿ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِۦ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُ ۚ وَمَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًۢا بَعِيدًا ﴿١١٦﴾ ﴾ [النساء : ١١٦].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Hakika Mwenyezi Mungu hamsamehe anayemshirikisha na Anamsamehe isiyokuwa shirki kwa anayemtaka}} [An-Nisaa : 116].

Enyi ndugu katika imani!Napenda kuchukua fursa hii kutaja mambo ambayo yanakwenda kinyume na Tawhidi. Mambo ambayo anatakiwa Muislamu ayajue na ajiepushe nayo baada ya kuyajua. Mshairi amesema:»Nimeijua shari si kwa ajili ya kuifanya, lakini kwa ajili ya kuiepuka na asiyejua kheri kutokamana na shari ataingia katika shari hiyo.»



www.global-minbar.com/sw

www.global-minbar.com/sw

## Mambo yanayo Haribu Tawhidi

Miongoni mwa mambo ambayo yanatakiwa ajitahadhari nayo yasije yakamtia katika matatizo dunaini na siku ya kiama. Miongoni mwa mambo hayo:-

- Ushirikina kwa aina zake zote. Kwani shirki kubwa inafutilia mbali imani. Na shirki ndogo ina punguza ukamilifu wa Tawhidi.Na mfano wa shirki ni kumuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu jambo ambalo hana uwezo nalo isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na katika shirki kubwa ambayo tunayaona leo ni kufanya tawaf kunyenyekea makaburi, kwenda kwa waganga na wachawi bali kuyaamini yote wanayoyasema kwa kudai mambo yaliofichika, na uhakika ni kwamba hakuna anayejuwa yaliofichika isipokuwa Mwenyezi Mungu na hakuna anayeweza kuleta madhara kumpata mtu isipokuwa Mwenyezi Mungu na hakuna anayeweza kuzuia kheri Akitaka Mwenyezi Mungu kuleta kheri hiyo.

قال تعالى : ﴿ وَإِن يَمْسَسْكَ ٱللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَ ۖ وَإِن يَمْسَسْكَ بِخَيْرٍ فَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٧﴾ ﴾ [الأنعام : ١٧].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Na Mwenyezi Mungu Akimpa mtu mtihani wa madhara (ugonjwa) hakuna Anayeweza kuuondoa isipokuwa yeye na akimpa neema (siha nzuri utajiri) hakuna awezaye kuiondosha kheri hiyo isipokuwa Mwenyezi Mungu}} [ Al-Anaam : 17]. Kwa hivyo, tujue ya kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye anayeleta manufaa na madhara, na kwa sababu hiyo yatakiwa Mwenyezi Mungu aogopewe haki ya kuogopewa.

- Na aina za shirki ni mtu kuomba dua kumuomba mtu jambo ambalo hakuna awezaye kulifanya isipokuwa Mwenyezi Mungu kama kuondoa ugonjwa. Huku tukijua ya kwamba dua ni ibada, kwa hivyo, ibada hiyo ya dua haifai kufanyiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu.
- Aina nyingine ya shirki kubwa ni ushirikina katika nia na makusudio, hii ni mtu kunuwia au kufanya ibada kwa kutaka au kukusudia mambo ya kidunia au wamuone kwamba yuwafanya ibada au watu wamsikie au apate sifa kwa watu.

قال تعالى : ﴿ مَن كَانَ يُرِيدُ ٱلْحَيَوٰةَ ٱلدُّنْيَا وَزِينَتَهَا نُوَفِّ إِلَيْهِمْ أَعْمَٰلَهُمْ فِيهَا وَهُمْ فِيهَا لَا يُبْخَسُونَ ﴿١٥﴾ أُو۟لَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ لَيْسَ لَهُمْ فِى ٱلْـَٔاخِرَةِ إِلَّا ٱلنَّارُ ۖ وَحَبِطَ مَا صَنَعُوا۟ فِيهَا وَبَٰطِلٌ مَّا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾ ﴾ [هود : ١٥ – ١٦].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Anayetaka uhai wa dunia na mapambo yake tutawapa malipo ya amali zao hapa duniani na hawatapunguziwa kitu, hao ni wale ambaye hawatakuwa na chochote kesho akhera isipokuwa moto na yatabatilishwa yote waliyoyafanya na ni batili yote ambayo walikuwa wakiyafanya}} [Huud : 15 - 16]. Haya ni malipo ya wanaofanya ibada kwa ajili ya kuonekana na watu na kwa ajili ya dunia.

- Aina nyingine ni shirki ya kutii viongozi wa dini kinyume na miongozo sahihi ya Uislamu katika kuhalalisha vilivyoharamishwa na Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

قال تعالى : ﴿ ٱتَّخَذُوٓا۟ أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَٰنَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ ٱللَّهِ ﴾ [التوبة : ٣١].

Amesema kuwatii wanaohalalisha vilivyoharamishwa: {{Wamewafanya

www.global-minbar.com/sw

wanavyuoni wao na wafanya ibada ni miungu kinyume}} [Tawba : 31]. Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) Alimfasiria Adiy bin Hatiim ibada yenu kwao ni kumtii katika kumuasi Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala).

## KHUTBA YA PILI

Shukrani za dhati zote zamstahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote. Rehma na amani zimfikie Kipenzi chetu Mtume Muhammad. Ama baada ya haya, napenda kuendelea kuzitaja aina za shirki nazo ni:

### Aina za Shirki:

- Aina nyingine ya shirki ni kumpenda mtu au kitu zaidi kuliko Mwenyezi Mungu tena katika hali ya kumtukuza au kukitukuza kitu kile na kukidhalilikia.Na pindi mapenzi haya yafanyiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu basi ni shirki.

قال تعالى : ﴿ وَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ ٱللَّهِ أَندَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ ٱللَّهِ ۖ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَشَدُّ حُبًّا لِّلَّهِ ۗ ﴾ [البقرة: ١٦٥].

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala): {{Na katika watu wanawafanya wasiokuwa Mwenyezi Mungu kuwa wanavyompenda Mwenyezi Mungu na hakika walioamini wanampenda zaidi Mwenyezi Mungu}} [Al-Baqara : 165].

Kueni ndugu katika imani kwamba ukubwa wa dhambi la shirki kwani Mwenyezi Mungu hamsamehe anayemshiriksha endapo atafariki na dhambi hizo bila kumtaka yeye msamaha kwa kuwa Mola (Subhaanahu wa Taala) haridhii isipokuwa Tawhidi na pia haisamehe shirki. Kwa hivyo, adhabu ya mshirikina ni kubwa na atapata udhalilifu hapa duniani kabla ya kuadhibiwa kesho akhera.

قال تعالى : ﴿ إِنَّهُۥ مَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ ٱللَّهُ عَلَيْهِ ٱلْجَنَّةَ وَمَأْوَىٰهُ ٱلنَّارُ ۖ وَمَا لِلظَّٰلِمِينَ مِنْ أَنصَارٍ ﴿٧٢﴾ ﴾ [المائدة: ٧٢].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Hakika mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu amemuharamisha pepo na makazi yake ni motoni na hawatapata madhalimu wenye kuwasaidia}} [Al-Maaidah : 72].

**Napenda tujiuze maswali yafuatayo;**

1. Ni nani katika sisi hataki usalama duniani na kesho akhera?
2. Ni nani kati yetu hataki kuingia peponi bila ya hesabu?
3. Ni nani kati yetu hataki kupata uhai mzuri duniani na kuokoka siku ambayo haitofaa mtu mali yake wala watoto isipokuwa atayenda kwa Mwenyezi Mungu kwa moyo uliyosalimika na madhambi?

Jawabu la maswali tuliyoyauliza kuitekeleza Tawhidi katika maisha yake yote. Kubwa linalotakiwa ni mtu kujifundisha mambo yanayofungamana na Tawhidi vizuri kuyatilia umuhimu mkubwa katika maisha yake kwa kusoma vitabu vya Tawhidi na kusikiliza darasa za wanavyuoni walioshikamana na Tawhidi na sunna, kwani kufanya hivyo ni nuru katika nyoyo. Na vile vile kuvisoma vitabu



www.global-minbar.com/sw

vya Tawhidi ili kujua Tawhidi ni nini Tawhidi,sababu za shirki,hukmu za shirki na dalili za hukumu za shirki hizo, kuyajuwa hayo ni mwangaza ili mtu asibaki katika giza la shirki, na Tawhidi pia hutengeneza moyo wa mtu na jamii kwa jumla.

Enyi ndugu katika imani! Msihadaike na dunia na kuipuuza Tawhidi iliyokusanya kila kitu na kila mafanikio duniani na kesho akhera na kwa ajili ya Tawhidi wametumlizwa Mitume wote na kuumbwa pepo na moto. Nawausia ndugu zangu Waislamu mulipe suala hili la Tawhidi kipaumbele katika maisha yetu, na muikabili Tawhidi kwa nia njema na nia ya kweli. Na haifai kulipuuza kwa hali yoyote kwani atayelipuuza suala hili yuko katika hatari kubwa duniani na vile vile kesho akhera.

## Mwisho

Twamshukuru Mungu tumegusia nukta muhimu kwa kubainisha umuhimu wa Tawhidi na kwamba Tawhidi ni sababu kubwa ya kuokoka mwanadamu siku ya kiama kupata msamaha pia tukabainisha kwamba Tawhidi ni sababu ya kuondoshewa balaa na fitna na mwisho tumebainisha umuhimu wa kujifundisha Tawhidi na shirki kwa aina zake.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Azitengeneze nia zetu katika vitendo vya kila siku na azitengeneze ibada zetu za kwa jumla, pia Aitengeneze Dini yetu na dunia yetu kwani yeye ni muweza wa kila kitu.

www.global-minbar.com/sw

www.global-minbar.com/sw

# [2] MAJINA MAZURI YA MWENYEZI MUNGU NA UFAFANUZI WAKE

## Lengo la Khutba:

1. Kuhimiza juu kuamini majina ya Mwenyezi Mungu.
2. Kufafanua baadhi ya majina ya Mwenyezi Mungu.
3. Kuhimiza kuomba dua kwa majina ya Mwenyezi Mungu.
4. Kubainisha majina ya Mwenyezi Mungu ni kwa mujibu wa Qur'an na Hadith za Mtume.

## KHUTBA YA KWANZA

## Utangulizi

Shukran ni za Mola wa viumbe vyote.Rehma na amani zimfikie Mtume Muhammad. Tutazungumzia katika khutba hii tukufu tutahimizana juu ya kuamini majina ya Mwenyezi Mungu pia tutafafanua maana ya baadhi ya majina ya Mwenyezi Mungu tutaendelea kuhimizana kuomba dua kwa majina ya Mungu vile vile tutaweka wazi ya kwamba majina ya Mwenyezi Mungu ni kulingana na Quran na hadithi za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).

Ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumtakia rehma na amani Mtume Muhammad. Ni lazima kwa kila Muislamu aamini kuweko kwa Mwenyezi Mungu na kuamini kuwa Mwenyezi Mungu Ndie Aliyeumba kila kitu na yeye ndiye Anayeupeleka ulimwengu na anafanya atakalo. Pia ni wajibu kwa Muislamu kuamini kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye anayestahiki kuabudiwa peke Yake kama ambavyo inatakiwa kwa Muislamu kuamini kwamba Mwenyezi Mungu hafanani na yoyote katika majina Yake na sifa Zake. Muislamu akiamini haya tuliyoyataja basi imani yake kwa Mwenyezi Mungu itakuwa imekamilika.

Enyi waja wa Mwenyezi Mungu munaonisikiliza, Hakika ni katika kumuamini Mwenyezi Mungu kuamini majina Yake mazuri na sifa zake tukufu bila ya kufananisha wala kuzipuuza.

قال تعالى : ﴿وَلِلَّهِ ٱلْأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ فَٱدْعُوهُ بِهَا﴾ [الأعراف : ١٨٠].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Mwenyezi Mungu Ana majina mazuri, muombeni kwa majina hayo}} [Al-Araaf : 180]. Katika maneno haya tunapata faida kwamba haifai kwa yoyote kubadilisha jina lolote au sifa yoyote ya Mwenyezi Mungu kwa sababu yoyote ile na pia haifai kufananisha jina au sifa ya Mwenyezi Mungu na jina au sifa ya mtu yoyote. Kwani kufanya hivyo ni kumfanya sawa Mwenyezi Mungu na kiumbe wake, Vilevile haifai kabisa kusema kwamba jina ambalo Mwenyezi Mungu Amelithibitisha au Mtume wake (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) jina hilo au sifa hiyo. Ni vyema kwa Muislamu ayajue majina ya Mwenyezi Mungu na amuombe kwa majina hayo.

www.global-minbar.com/sw

www.global-minbar.com/sw

## Misingi Muhimu ya Majina na Sifa za Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)

Ndugu katika imani! Nafurahi kukutajia baadhi ya misingi inayohusiana na majina hiyo;

1. Majina ya Mwenyezi Mungu yote ni mazuri tena yamefikia kilele katika uzuri kwa kule kukusanya kwake sifa zilizokamilika zisizo na upungufu ndani yake kwa namna yoyote.

   قال تعالى : ﴿وَلِلَّهِ ٱلْأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ فَٱدْعُوهُ بِهَا﴾ [الأعراف : ١٨٠].

   Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Mwenyezi Mungu Ana majina mazuri, muombeni kwa majina hayo}} [Al-Araaf : 180].

2. Majina ya Mwenyezi Mungu ni yale aliyojiita kwa majina hayo au aliyomwita yeye Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) na haifai kwa mtu yoyote kutunga jina na kumpa Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala). Inavyotakiwa ni mtu kumwita Mwenyezi Mungu majina aliyojiita Mwenyewe katika kitabu chake na yale ambayo Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) katika hadithi zake tukufu, wala hafai mtu kuzungumza jambo bila ya ujuzi.

   قال تعالى : ﴿وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِۦ عِلْمٌ﴾ [الإسراء : ٣٦].

   Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Asema: {{Wala usizungumze jambo ambalo huna ujuzi nalo, hakika masikio na macho na moyo kutaulizwa kuhusiana navyo}} [Al-Isra : 36].

3. Majina ya Mwenyezi Mungu hayana idadi maalumu. Muislamu atakiwa alijue hili vizuri kabisa, na hii ni kwa mujibu wa hadithi ya Mtume (Swalla Llahu ‘alayhi wasallam) aliposema: [ Ewe Mwenyezi Mungu na kuomba kwa kila jina ambalo liko kwenye kitabu chako, au ulilomfundisha yoyote katika viumbe vyako, au ulilolificha katika elimu isiyojulikana na yoyote kwako]. Katika majina ambayo Mwenyezi Mungu hakuyataja wala hakuyafundisha viumbe nakuonesha kwamba majina yake hayana idadi maalumu.

   Baada ya kutaja misingi muhimu ambayo yatakiwa kwa Muislamu aifahamu vizuri ili imani yake kwa Mwenyezi Mungu hususan katika majina yake na sifa zake iwe imekamilika vyema.

## Maana ya Majina ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala)

Nachukua tena nafasi nyengine kufafanua baadhi ya majina ya Mwenyezi Mungu. Na katika majina hayo ni:-

1. (ALLAH ) ni muabudiwa wa haki kwa mapenzi yote katika ibada hiyo katika hali ya kumtukuza.
2. (MWINGI WA REHMA MWENYE KUREHEMU) ni Ambaye anawahurumia zaidi waja wake kuliko mzazi kumhurumia mwanawe, kwani neema yoyote inayopatikana ni kwa huruma ya Mwenyezi Mungu na hakuna dhara lolote lililomuepuka mwanadamu, pia ni kwa rehma ya Mwenyezi Mungu.

www.global-minbar.com/sw

قال تعالى : ﴿ وَمَا بِكُم مِّن نِّعْمَةٍ فَمِنَ اللَّهِ ﴾ [النحل : ٥٣].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Na hakuna neema yoyote isipokuwa yatoka kwa Mwenyezi Mungu}} [An-Nahal : 53].

3. (MFALME) Mwenye kumiliki ulimwengu wote juu yake na chini kiasi kwamba hakitikisiki chochote isipokuwa Anajua bali yeye Ndiye Aliyetaka kitikisike.

قال تعالى: ﴿ مَٰلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٤﴾ ﴾ [الفاتحة : ٣].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Mfalme siku ya malipo}} [Al-Faatiha : 3].

4. (MTAKATIFU) ni aliyetakasika na upungufu waliyonao viumbe vyake, kwani Mwenyezi Mungu hapatwi na uchovu wala maafa yoyote kinyume na mwanadamu hupatwa na machovu na pia maafa.

قال تعالى : ﴿ وَلَقَدْ خَلَقْنَا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَمَا مَسَّنَا مِن لُّغُوبٍ ﴿٣٨﴾ ﴾ [ق : ٣٨].

Amesema Mola (Subhaanahu wa Taala): {{Na hakika si lingine tumeziumba mbingu na ardhi zilizo kati yake na hatukupatwa na uchovu}} [Qaaf : 38].

5. (MWENYE NGUVU MTENDESHA NGUVU) hakuna kiumbe chochote isipokuwa kiko chini ya uwezo Wake pia kinamyenyekea Yeye.

قال تعالى : ﴿ مَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٧٤﴾ ﴾ [الحج : ٧٤].

Mola (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Na hawakumjua Mwenyezi Mungu haki ya kumjua hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Asiyeshindwa na yoyote}} [ Al-Hajj : 74].

6. (MJUZI) ni Ambaye yuwajua siri na kilichodhihiri na anajua kilicho bara na baharini na anajua kila kitu Ametakasika Mwenyezi Mungu.
7. (MTUKUFU ALIYE JUU) Aliye juu kwa dhati Yake juu ya Arshi na pia ni Mtukufu kwa sifa zake.
8. (ANAFANYA ATAKALO) Mwenye uwezo wa hali ya juu wa kufanya lolote analolitaka.
9. (MWENYE KUSAMEHE) Anayesamehe makosa yote aliyotendewa na anayesitiri aibu hata zikiwa nyingi kiasi gani. Amesema Mola katika Hadithi Qudsi: [ Ewe mwanadamu, hakika yako wewe utakachoniomba na ukatarajia basi nimekusamehe dhambi zote wala sijali].
10. (MWENYE HEKIMA) Anayeweka vitu pahali pake na anayekadiria vitu vizuri.
11. (MWENYE KUJITOSHELEZA) Anayejitosheleza mwenyewe asiyehitajia yoyote katika viumbe. Majina haya ndio nimeona niwafafanulie kwa uchache lakini majina mengine mengi ya Mwenyezi Mungu nimeyaacha kulingana na wakati

Enyi waumini, mnaonisikiliza! yamekuja mahimizo makubwa juu ya kuomba dua kwa majina ya Mwenyezi Mungu.

www.global-minbar.com/sw

قال تعالى : ﴿وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَاۖ﴾ [الأعراف : ١٨٠].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Mwenyezi Mungu Ana majina mazuri, muombeni kwa majina hayo}} [Al-Araaf : 180]. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) amebainisha namna gani tutamuomba Mwenyezi Mungu kupitia majina yake matukufu. Katika hadithi Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alimsikia mtu katika maswahaba akisema: [Ewe Mwenyezi Mungu, Nakuomba wewe kwani sifa na shukrani zote ni zako, hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe peke yako. Huna mshirika, Mwenye kusimulia unalofanya, Muumba wa mbingu na ardhi, Mwenye utukufu, na ukarimu, Ewe ulio hai Mwenye kusimamia kila kitu. Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) akasema: " Hakika umemuomba Mwenyezi Mungu aliyetukuka kwa jina lake tukufu ambalo akiombwa kwa jina hilo hujibu na Akiombwa hutoa]. Kwa hivyo, ni juu yako mja wa Mwenyezi Mungu kuomba kwa majina yake.

Amesema Sheikh Muhammad Swaleh Uthaimin Allah Amrehemu katika kubainisha maana ya Neno lake Mwenyezi Mungu: "Muombeni kwa majina yake". Amesema Sheikh: 'Ni kuyafanya ni njia ya kupata unachotaka katika maombi, kwa hivyo, utachagua jina linalonasibiana na matakwa yako, kwa mfano ikiwa unaomba msamaha basi utasema: "Ewe Mwenye kusamehe nisamehe". Na hainasibiani kusema: " Ewe Mwenyezi Mungu Mkali wa kuadhibu nisamehe, bali hii ni kama kumcheza Mwenyezi Mungu shere, na inatakiwa useme «Ewe Mwenyezi Mungu Mkali wa adhabu niepushie adhabu Yako'.

Ndugu Waislamu, kinachotakiwa kwetu ni kukitegemea zaidi kitabu cha Mwenyezi Mungu na hadithi za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) katika kuyajua majina ya Mwenyezi Mungu, kwani haifai kabisa kwa yoyote kumpa Mwenyezi Mungu jina ambalo hakujiita jina hilo wala hajamuita jina hilo Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam).

## KHUTBA YA PILI.

Shukrani za dhati na sifa njema zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu Mola wa mashariki na magharibi. Rehma na amani zimfikie Kipenzi chetu na kiongozi wetu Mtume Muhammad. Ama baada ya kumtukuza Mwenyezi Mungu na kumsifu kwa sifa zake Anazostahiki kusifiwa nazo na kumtakia rehema na amani Mtume wetu mkarimu.

Napenda kuchukua fursa nyingine katika khutba hii kuzitaja baadhi ya dua ambazo Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alizoomba kwa majina mazuri ya Mwenyezi Mungu. Mtume asema: [ Ewe Mwenyezi Mungu wewe ni Mola wangu hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki ila wewe umeniumba na mimi ni mja wako na niko katika dhamana yako na ahadi yako niwezavyo, narudi kwako kwa neema zako kwangu, na nirudi kwako na dhambi zangu, basi nisamehe, kwani hasamehe dhambi isipokuwa wewe. Najilinda kwako kutokamana na shari ya kila nilichofanya]. Na akasema Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam): [ Mwenye kusoma dua hii wakati wa usiku na akafa usiku huo, basi ataingia peponi].

www.global-minbar.com/sw

www.global-minbar.com/sw

Na Mtume alipokuwa akiswali alikuwa akisema: [Nimeuelekeza uso wangu kwa yule Aliyeumba mbingu na ardhi hali kujiepusha na shirki na hali ya kuwa mimi ni Muislamu na sikuwa katika washirikina. Hakika swala yangu na ibada zangu za kuchinja, na uhai wangu na kufa kwangu ni kwa Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, hana mshirika na kwa hili nimeamrishwa na mimi ni Muislamu wa kwanza. Ewe Mwenyezi Mungu, Wewe ni Mfalme hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe, Wewe Mola wangu na mimi ni mja wako nimejidhulumu nafsi yangu, na nimezikubali dhambi zangu zote, kwani hakika hasamehe dhambi isipokuwa wewe. Niongoze katika tabia njema, kwani hakuna mwenye kuongoza katika tabia njema ila Wewe, na uniondoshee tabia mbaya kwani hakuna mwenye kuondosha tabia mbaya ila Wewe. Nakuitikia wewe, na utukufu ni wako na kheri zote ziko mikononi mwako na shari haitegemezwi kwako. Mimi niko kwako, umetukuka na umetakasika. Nakutaka msamaha na narudi kwako].

Na Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa akisema wakati akirukuu: [ Ewe Mwenyezi Mungu nimerukuu kwa ajili yako na nimekuamini Wewe na kwako Wewe nimjisalimisha na yamenyenyekea kwako masikio yangu, macho yangu, akili yangu, mifupa yangu na mishipa yangu]. Pia Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa akisema anapoinuka kutoka kwenye rukuu: [ Mwenyezi Mungu Amemsikia Anayemsifu, Mola wetu, shukran ni zako wewe zilizomo mbinguni na ardhini na baina yake na katika kila kitu baada yake].

Vilevile Mtume alikuwa akisema katika sijida: [ Ewe Mwenyezi Mungu, ni mesujudu kwa ajili yako na nimekuamini wewe na nimejisalimsha kwako, umesujudu uso wangu umsujudu Aliyeumba na Akautia sura na akapasua masikio yake na macho yake. Basi Ametakasika Mwenyezi Mungu Mbora wa kuumba]. Na akimaliza kuswali anasema: [Ewe Mwenyezi Mungu, Nisamehe mimi madhambi niliyoyatanguliza na niliyoyachelewesha na niliyoyafanya kwa siri na niliyofanya kwa dhahiri na niliyoyafanya kwa wingi na unayoyajua wewe zaidi kuliko mimi. Wewe ni Mwenye kumtanguliza umtakaye, na Mwenye kumweka nyuma umtakaye, hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila wewe].

Enyi waumini wa kweli! jiepusheni na kumuita Mwenyezi Mungu majina yasiyokuwa yake bila ya ujuzi, kwani kufanya hivyo ni kuzungumza juu ya Mwenyezi Mungu bila ya elimu.

قال تعالى : ﴿وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِۦ عِلْمٌ﴾ [الإسراء : ٣٦].

Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa Taala) Amesema: {{Wala usizungumze jambo ambalo huna ujuzi nalo}} [Al-Isra : 36].

Mwisho napenda kukariri kwa kuhimiza kuyaamini majina ya Mwenyezi Mungu na kufanya vitendo ambavyo vinalingana na imani hiyo.

Enyi waumini mcheni Mwenyezi Mungu na mjue ya kwamba mnaelekea kwake, na shikamaneni na kitabu chake na mushikamane na sunna sahihi za Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam), na mumuite Mwenyezi Mungu kwa majina yake Aliyejiita, na sifa zake alizojisifu nazo, na atakaye kwenda kinyume

na maamrisho yake,  basi Mwenyezi Mungu Amemuahidi adhabu kali.

## Mwisho

Kwa kweli tumezungumzia kuhusu kuhimizana juu ya kuamini majina ya Mungu pia tukafafanua maana za baadhi ya majina ya Mungu vile vile tukahimiza kuomba dua kwa majina ya Mungu kama ambavyo tumeweza ya kwamba majina ya Mungu ni kulingana na Quran na hadithi za Mtume rehma na amani zimfikie.

Mwisho kabisa tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaaliye tuwe miongoni mwa wenye kusikiliza yaliomema na tuwe ni wenye kuyafuata.Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe imani iliyothibiti na aturuzuku matendo mazuri. Amin!

www.global-minbar.com/sw